

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ حَامَوْا مِنْكُمْ وَعَيْلُوا الصَّلَاحَ دِيْنَهُمْ لِيَسْتَخْلِفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْتُمْ تَخْلُفُنَّ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُمْ دِيْنٌ إِذْنَنِ اللَّهِ أَرْغَفَنِهِمْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقَهِمْ أَنَّهُ
يَصْدُورُونِي لَا يُشْرِكُونِي فِي شَيْءٍ وَمَنْ كَفَرَ بِهَذَهِ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ



Na: 09 / 1446 H

Jumapili, 20 Jumada II 1446 H

22/12/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo vy'a Habari
Mfano Hatari Ambao Haupaswi Kupuuzwa
(Imetafsiriwa)**

Katika mfano hatari katika historia ya mapinduzi, Huduma Kuu ya Usalama mjini Aleppo iliteka nyara wanawake kumi mnamo siku ya Jumamosi, 21 Disemba 2024. Wanawake hao walikuwa wamejitokeza wakiandamana, wakitaka utawala wa Uislamu na kuachiliwa huru waume zao, vijana wao na watoto wao waliotekwa nyara zaidi ya mwaka mmoja na nusu uliopita. Watu hawa wamefungwa jela na Jolani [al-Julani] mjini Idlib tangu Mei 7, 2023!

Tunawahutubia watu wote wa mapinduzi na wanaharakati miongan mwao, wakiwemo wapiganaji, wanafunzi, wataalamu wa vyombo vy'a habari, wasomi, na mashirika: Je, mapinduzi haya, pamoja na kujitolea muhanga na mamilioni ya waliokufa mashahidi na watu waliohamishwa makaazi yao, yalizinduliwa kwa ajili ya hili? Jel ilikuwa ni kwa vitendo kama hivyo, kuiga yale ambayo utawala wa kihalifu wa Assad ulifanya kwa miongo kadhaa?

Ni kinaya kwamba huku wanawake wasiokuwa na hijab jijini Damascus wanaweza kuandamana kwa uhuru kwa ajili ya usekula na uhuru bila mtu ye yeyote kuwaingilia, wanawake wema wanaotaka kutekelezwa kwa Shariah ya Mwenyezi Mungu na kuachiliwa huru kwa vijana wao ambao wametekwa nyara kwa muda wa mwaka mmoja na nusu wangali wametekwa nyara!

Enyi Watu wa Mapinduzi, mlajitolea muhanga na kuvumilia mengi: Je, mapinduzi haya hayakuanza ili kulinda heshima ambayo utawala dhalimu wa Assad ulikuwa umekiuka? Je, sasa tunaweza kukubali kuregeshwa kwa sera kama hizo, zinazolenga wanawake wema?

Mapinduzi ya Al-Sham yalichochewa na kauli moja ya mhalifu Atef Najeeb, ambapo aliwatukana wanawake waheshimiwa wa Daraa. Leo, tunashuhudia kutekwa nyara kwa wanawake wema katika hatua ya kwanza ya usalama baada ya kuanguka kwa utawala wa kihalifu. Jihadharini na kukaa kimya juu ya vitendo kama hivyo, kwani heshima ni mstari mwekundu, ambao maisha hutolewa kafara, na kila rasilimali ya thamani hutumiwa.

Enyi Watu wa Mapinduzi, je, mtakubali kwamba wanawake kumi waliotaka kuondolewa dhulma waliyotendewa, watekwe nyara huku wanawake walio bila ya hijab, ambao mwanzoni walitoa wito wa kuuwawa watoto na wanawake, wanaruhusiwa kuandamana kwa uhuru? Na wapi? Jijini Damascus, jiji la Bani Umayya, na katika uwanja ulioitwa kwa jina lao!

Mcheni Mwenyezi Mungu kwa heshima yenu, ambayo kwayo mliibuka katika mapinduzi. Jihadharini na kukaa kimya, kwa maana matokeo yake ni makubwa, na majuto yatakuja wakati mushachelewa.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Syria**